SALAMU ZA CHAMA CHA WAAJIRI TANZANIA (ATE) KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI, 28-4-2019, MBEYA

Mh. Jenista Mhagama (Mb) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu,

Bi. Hadija Mwenda, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA),

Bw. Tumaini Nyamhokya- Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),

Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya,

Mh. Anthony Mavunde (Mb) na Naibu Waziri, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu,

Mh. Stella Ikupa (Mb) na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Watu wenye Ulemavu,

Bw. Jealous Chirove, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani Ofisi ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi,

Dkt. Yahya Msigwa-Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),

Ndugu Waandishi wa Habari,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Itifaki imezingatiwa!

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dkt Aggrey Mlimuka ambaye angependa kuwepo hapa leo lakini kutokana na sababu zisizoweza kuzuilika amenituma nisome salamu hizi za ATE katika maadhimisho haya muhimu.

Chama cha Waajiri Tanzania kinatoa shukrani kwa kamati ya maandalizi kwa kuandaa maadhimisho haya yenye kauli mbiu isemayo **"Usalama na Afya na Mustakabali wa Kazi kuelekea Uchumi wa Viwanda".** Maadhimisho haya yanatoa fursa kwa wadau wa masuala ya usalama mahali pa kazi kuweza kukutana.

Nipende kuishukuru Serikali kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Mh Jenista Mhagama ambaye ameweza kuhudhuria hapa leo. Mh tunakushukuru sana na tunaishukuru Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kudumisha ushirikiano uliopo. Jambo hili la afya na usalama mahali pa kazi ni muhimu kwa ustawi wa wafanyakazi wetu ambao ni nyenzo muhimu sana katika uzalishaji wa bidhaa na huduma. Wafanyakazi wanatoa nguvukazi ambayo inatumika kufanya uzalishaji wa bidhaa na huduma na endapo wakitumika vizuri tutasukuma maendeleo ya uchumi wetu mbele.

Mh Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana

Tunaishukuru Serikali kwa kufanyia kazi mapendekezo ya kupunguza gharama za tozo za OSHA, kwa mfano katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilifuta baadhi ya tozo ili kupunguza gharama na kuboresha mazingira ya kufanya biashara kama ifuatavyo:-

- Kupunguza ada ya fomu ya usajili ambayo ilikuwa shilingi 2000 kwa lengo la kupunguza gharama,
- kufuta ada ya usajili wa maeneo ya kazi kwa kuzingatia ukubwa wa eneo ambayo ilikuwa ikitozwa kwa kiasi cha shilingi 50,000 hadi 1,800,000 kulingana na eneo hivyo usajili kwa sasa ni bure
- imefuta ada ya Leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi iliyokuwa ikitozwa Tshs 200,000

Mh Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana,

AFYA NI MALI ni dhana ya kweli na naomba sasa nieleze maoni ya Waajiri kuhusu umuhimu wa Usalama na Afya kazini na namna gani itasaidia kuimarisha Uchumi wa Viwanda.

- Wafanyakazi ndio nyenzo muhimu inayotumika kusimamia nyenzo nyingine za uzalishaji kama ardhi (ambayo inahusisha raslimali zote za asili kama maji, miti, madini, wanyama na malighafi nyingine za kiasili) na mtaji au teknolojia mbalimbali.

- Wafanyakazi wakifanya kazi katika mazingira yaliyo bora watapata morali na motisha zaidi katika utendaji kazi wao na hivyo kuongeza ufanisi katika operesheni za kiwanda au shirika husika.
- Uendelevu wa kazi na uzalishaji utaimarika endapo wafanyakazi hawapati hatari ya kupata madhara ya kiafya au kifo mahali pa kazi- matumaini ya kufanya kazi mahali salama wakati wote yataongeza uendelevu wa kazi.
- Mazingira yenye usalama na afya yatapungiza gharama za kioperesheni kwa wenye viwanda kwa sababu ya kupungua gharama za dharula na matibabu. kutaongeza faida za kibiashara na kuhamasiha uwekezaji Zaidi katika viwanda.
- Usalama na afya mahali pa kazi utahamasiha kutunza wafanyakazi muhimu wenye vipaji kwani watafurahia kufanya kazi na muajiri au kiwanda ambacho kinatoa kipaumbele kwenye afya na usalama wao.

Mh Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana,

Pamoja na faida hizo hapo juu bado zipo changamoto zinazokwamisha uimarishaji wa Usalama na Afya mahali pa kazi kama ifuatavyo:-

- Uelewa mdogo wa baadhi ya Waajiri/ wenye viwanda hususani kuhusu umuhimu wa kuhakikisha kunakuwepo Usalama na Afya mahali pa kazi.
- Waajiri au wenye viwanda wengi wanaona kwamba uwekezaji wenye usalama na afya mahali pa kazi ni gharama sana na wengi huionekana hawajajiandaa kwa ajiri yakufanya maboresho yanayopaswa kufanywa.
- Kuendelea kwa matumizi ya teknolojia zisizo rafiki kwa afya za wafanyakazi kwa mfano mitambo inayoharibu uoto wa asili ambao unatengemneza hewa safi inayoleta utulivu nakuongeza ufanisi wa wafanyakazi.
- Kutokufata sheria na viwango vya kazi zenye staha baina ya Waajiri walio wengi na kuongezeka kwa maonjwa ya aina mbalimbali hususani yale ya kitropiki kama malaria, kipindu pindu, pamoja na kifua kikuu. Usaambaaji wa magonjwa haya unakwaza udhibiti na uhakikikishaji wa mazingira bora na rafiki kwa wafanyakazi

Mh Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana

Upo mchango ambao Waajiri tunaweza kufanya katika kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi utakaofanikisha uendelevu wa uchumi wa **viwanda**. Waajiri wanaweza kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuwekeza katika kutoa elimu na vifaa na namna bora za wafanyakazi kujilinda dhidi ya hatari za kiafya na usalama wao mahali pa kazi.
- Kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa na uelewa mzuri wa namna vifaa na mifumo mbali mbali inavyofanya kazi ili kuzuia na kudhibiti hatari mbali mbali zinazoweza kujitokeza. Pia kuhakikisha kila mfanyakazi anaelimishwa kuhusu

magonjwa mbali mbali ambayo anaweza kuyapata mahali pa kazi mna njia za kuyaepuka.

Mh Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana

Nchi yetu itaweza kufanikiwa kupata faida za mazingira bora ya kufanya kazi kwa wafanyakazi tunapoelekea kufanikisha uchumi wa viwanda endapo tuendeleza mahusiano na mashirikiano yaliyopo kati ya Serikali, sekta binafsi, asasi mbali mbali zisizo za kiserikali katika kufanya utatuzi wa changamoto zilizopo katika kutoa elimu na uhamasishaji, kuwekeza rasirimali zetu ili kuhakikisha kuwa mahali pa kazi hususani katika viwanda kuna Usalama na Afya.

Tunaiomba Serikali iendelee kutatua changamoto mbalimbali zitokanazo na utekelezaji Usalama na Afya kazini ili kuchochea ustawi wa wafanyakazi wetu na kupunguza gharama za kufanya biashara ndani ya nchi yetu ili hatimaye tufikie malengo ya kufikia uchumi wa kati uliojengwa na viwanda.

Asanteni Sana kwa kunisikiliza